



**MWITO KWA WASHIKADAU WOTE WA MABADILIKO YA ANGA NCHINI KENYA**

Wizara ya Mazingira na Mali Asili (MEMR) imo katika harakati za kutekeleza Mpango wa Marekebisho barani Afrika (Africa Adaptation Programme-AAP) kwa ufadhili wa Serikali ya Japan, kupitia Mpango wa Ustawi wa Mataifa (UNDP). Lengoku kuu la AAP ni kuelekeza Kenya katika ustawi mkuu kuhusiana na mabadiliko ya hali ya anga kwa kuimarisha uwezo na uongozi wa mifumo na taasisi ili kukabiliana na hatari na nafasi zinazotokana na mabadiliko ya anga kupitia kwa mkakati wa kitaifa kuhusu marekebisho. Mabadiliko ya hewa ni mojawepo wa vitisho vikuu kwa jitihada za Kenya kufikia mbinu za ustawi – Ruwaza ya 2030 na Malengo ya Ustawi ya Milenia (MDGs), na lazima nchi hii iungane katika jitihada zake za kukabiliana na vitisho hivyo.

AAP na Afisi Kuu ya Mabadiliko ya Anga (MEMR) ziko katika harakati ya kubainisha na kupambanua vihusika katika mabadiliko ya hewa humu nchini. Hatua hii itapelekea kuundwa kwa hifadhi ya habari ambayo itaimarisha mtandao wa ufahamu kuhusu mabadiliko ya anga. Kadhalika, hifadhi hiyo itaimarisha upatikanaji wa maarifa, mienendo, teknolojia bunifu na nafasi nyinginezo kwa manufaa ya umma kwa jumla na hata jamii ya kimataifa, ambayo itachangia katika uimarishaji wa nguvu dhidi ya athari za mabadiliko ya anga. Tunatoa mwito wa ushirikiano na kila mmoja wetu nchini Kenya ambaye amejishughulisha na shughuli ambazo zinachangia kujirekebisha kulingana na mabadiliko ya anga au upunguzaji wa mabadiliko hayo ili kufanikisha jitihada za hifadhi iliyopendekezwa kwa kuimarisha habari zifuatazo:

**Jina la shirika**

**Eneo la kikazi (ajira)** k.m. kilimo/ufugaji, kawi, maji au udhibiti wa mikasa, usimamizi wa mali asili, maji taka, biashara ya carbon/kulipia huduma za kimazingira, sera za kitaifa na mipangilio, n.k.

**Anwani ya mradi**

**Onyesha iwapo mbinu zako ni: marekebisho/ uzuiaji/ utetezi n.k.**

**Mienendo mizuri/matokeo muhimu/mafunzo**

**Aina ya rasilimali zilizopo,** k.m. Data kuhusu anga, utafiti/vitabu, vifaa, mradi/jitihada, jaribio la utafiti, kongamano/vifaa vya kufundishia

**Mfadhili na kiasi cha bajeti**

**Aina ya msaada uliopatikana (kifedha/kiufundi)**

**Mahali pa kuendeshea shughuli/kata/jimbo/kitaifa**

**Waliolelengwa kunufaika** – mjini/mashambani/jinsia (Onyesha idadi pakihitajika)

**Idadi na Kiwango cha elimu cha Wataalamu wa Kiufundi kuhusu Mabadiliko ya Anga na Nyanja zao za utaalamu**

**Uhusiano/Muingiliano**- Onyesha washirika katika shughuli zilizotekelezwa na nambari zao za mawasiliano

**Njia ya mawasiliano** – Hasa – simu, kipepesi, barua pepe, mtandao

**Tunatarajia habari hizi kutoka kwa:**

Taasisi za Elimu na Utafiti, Mashirika ya serikali/Mashirika yasiyokuwa ya kiserikali (NGOs), Mashirika ya Kidini, NGOs za Kimataifa, idara za Serikali, sekta ya kibinafsi, miungano, makundi ya kijamii, watu binafsi, vyombo vya habari, miongoni mwa wengineo.

**Tafadhali wasilisha wasifu wa shirika lako kufikia tarehe 25 Machi, 2011 kwa:**  
[secretariatcc@environment.go.ke](mailto:secretariatcc@environment.go.ke) NA [info.aapkenya@gmail.com](mailto:info.aapkenya@gmail.com)

Africa Adaptation Programme (K)  
AAP Kenya Office  
Simu: +254 20 2327359

Anwani ya Mahali: Kenya Meteorological Department,  
National Meteorological Library, 1st Floor  
S.L.P. 30259 – 00100,  
Nairobi, Kenya

Imefadhiliwa na:

